MINISTÈRE
DE L'EUROPE
ET DES AFFAIRES
ÉTRANGÈRES

*Liberté*
*Égalité*
*Fraternité*

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

———

SOUS-DIRECTION DE L'ATTRACTIVITÉ ET DES RECRUTEMENTS

———

Bureau des concours et examens professionnels

# Concours externe, concours interne et troisième concours pour l'accès à l'emploi de secrétaire des affaires étrangères (cadre d'Orient) au titre de l'année 2026

**Épreuve écrite d'admissibilité n°4**

Mercredi 26 novembre 2025

## Swahili

## Section Afrique

Durée totale de l'épreuve : 3 heures - Coefficient : 3
*Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.*
Dictionnaire autorisé

Réponses courtes, dans la langue choisie au moment de l'inscription, à des questions à partir d'un dossier composé dans cette même langue permettant d'apprécier les connaissances linguistiques et l'aptitude à formuler des réponses complexes sur les sujets d'actualité en lien avec la section choisie.

Ce dossier comporte 5 pages (page de garde, sujet et sommaire non compris).

## Sommaire


Document 1 ........................................ 1
Document 2 ........................................ 2
Document 3 ........................................ 3
Document 4 ........................................ 4
Document 5 ........................................ 5

## Questions

### Question 1 (7 points) :

Je, sera ya kurejesha kazi za sanaa za kiafrika kwa nchi za Afrika inaleta faida gani?

### Question 2 (7 points) :

Ufaransa inawezaje kujenga uhusiano mzuri na wa kudumu na nchi za Afrika, na kwa nini hii ni muhimu?

### Question 3 (6 points) :

Je, lugha ya kiswahili ina nafasi gani katika kukuza tamaduni za kiafrika duniani ?

## Document 1

### Je, ni nchi gani zinashikilia vitu vya kale vya nchi nyingine?

*BBC Swahili, 10 Disemba 2023*
*https://www.bbc.com/swahili/articles/c0j2xwvpk4eo*

Nchi za Ulaya zilipojenga himaya zao za kikoloni kote ulimwenguni, zilipata vitu vingi vya thamani ambavyo sasa vinaonyeshwa kwenye makumbusho ya nchi hizo.

**Vinyago vya Benin**

Vinyago vya Benin ni maelfu ya sanamu za chuma na mapambo mengine, yaliyoundwa kati ya karne ya 15 na 19. Mwaka 1897 majeshi ya Uingereza yalipora vinyago hivyo walipovamia na kuiharibu Benin, Nigeria ya sasa.

Vingi kati vinyago hivyo viliuzwa katika minada ya London na vingine vilinunuliwa na wakusanyaji wa kazi za sanaa kutoka nchi mbali mbali.

Tume ya Kitaifa ya Makumbusho ya Nigeria imetoa maombi rasmi kwa makumbusho kote ulimwenguni kurejesha sanamu hizo za shaba.

Novemba 2022, Jumba la Makumbusho la Horniman la London lilikubali kukabidhi vitu vya kale 72, vikiwemo vinyago vya shaba vya Benin.

Mwezi uliofuata, Chuo Kikuu cha Cambridge kilikubali kurudisha vinyago 116, na Ujerumani ikarudisha vitu vya kale 22.

Kuanzia 2026, vitu vya kale vitaonyeshwa katika Makumbusho ya Edo ya Sanaa ya Afrika Magharibi katika Jiji la Benin.

Vinyago vingine vya shaba vipo katika majumba za Uingereza, likiwemo British Museum, ambalo linahifadhi mkusanyiko mkubwa zaidi wa vitu vya kale vya Benin, takribani mia tisa.

Jumba hilo linasema Sheria ya Makumbusho ya Uingereza ya 1963 inazuia vitu hivyo kurudishwa.

## Document 2

### Je ni vitu vingapi ambavyo sasa vipo katika makumbusho tofauti duniani?

*BBC Swahili, 9 Disemba 2019*
*https://www.bbc.com/swahili/habari-50662077*

Nchini Ufaransa, rais Macron ameagiza kurudishwa kwa vito vya Afrika barani Afrika katika kipindi cha miaka michache ijayo.

Katika hafla moja iliofanyika mji mkuu wa Senegal Dakar, taifa hilo lilirudisha chombo kimoja- upanga uliokuwa ukimilikiwa na Omar Saidou Tall, ambaye alitawala maeneo ambayo yanajulikana kama Guinea , Senegal na Mali katika nusu ya pili ya karne ya 19.

Kwa sasa upanga huo umewekwa katika jumba la makumbusho la ustaarabu wa watu weusi katika mji mkuu wa Senegal Dakar.

Wakati wa ukoloni huko Afrika, maelfu ya mabaki ya vitu vya kale vilivyoibwa kwa sasa vinaoneshwa katika makumbusho ya Ulaya.

Lakini kuna baadhi ya taasisi ambazo zimekubali kurejesha vitu hivyo vya kale.

Kati ya asilimia 80 na 90 ya vitu vya makumbusho ya Afrika vipo kwenye makumbusho za kigeni, kulingana na ripoti rasmi ya Ufaransa iliyotolewa mwaka jana.

Inakadiriwa kuwa angalau karibia vitu vya kale 90,000 vilivyochukuliwa katika nchi za Afrika, hususan, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, zipo kwenye makumbusho ya Ufaransa.

Makumbusho ya Quai Branly nchini Ufaransa pekee inasemekana kuwa na vitu vya kale 46,000 vilivyochukuliwa kimabavu.

Tangu ripoti hiyo ilipotolewa, baadhi ya vitu vya kale vilivyoibwa vinatarajiwa kurejeshwa kutoka nchi za Ulaya hadi vilikotolewa ikiwemo vitu vya kale 26 vilivyochukuliwa nchini Benin, magharibi mwa Afrika enzi za ukoloni na kupelekwa katika makumbusho ya Quai Branly.

## Document 3

### Chifu Mkwawa alipinga utawala wa kikoloni Afrika mashariki

*BBC Swahili, 28 Juni 2019*
*https://www.bbc.com/swahili/habari-48796666*

Fuvu la Chifu Mkwawa limewekwa ndani ya sanduku la kigae katika jumba la ukumbusho la Mkwawa huko Kalenga, Tanzania ya kati.

Awali lilitundikwa katika nyumba ya afisa wa kikoloni huko Bagamoyo, kabla ya kuondolewa na kupelekwa Ujerumani - mkoloni wa mji huo - mwanzo mwa karne ya 20.

Fuvu hilo lilitumika kuwatishia Wahehe, ambao waliongozwa na shujaa huyo katika vita vya kupinga utawala wa kikoloni wa Ujerumani.

Lakini kwanini fuvu la shujaa huyo aliyepinga utawala wa kikoloni linatajwa katika 'Treaty of Versailles'?

Katikati ya maagizo kutoka Ufaransana Ubelgiji kuna kifungu cha 246 kisemacho: "Katika miezi sita... Ujerumani itarudisha kwa serikali ya ufalme wa Uingereza fuvu la Sultan wa Mkwawa, lililoondoshwa kutoka himaya ilokuwa chini ya utawala wa Ujerumani Afrika mashariki na kupeleka nchini Ujerumani."

Hatahivyo, fuvu hilo halikurudishwa katika miezi sita - ilichukua miaka 35 kwa hilo kufanyika.

Kwa hivyo ilipogunduliwa kuwa fuvu hilo lipo katika mji wa Bremen Ujerumani katika miaka ya 1950, gavana wa Uingereza wa iliyokuwa Tanganyika, Edward Twining, alikuwa mwepesi kuchukua hatua.

Lilitumika kama kiashiria cha Tanzania ilio huru na inayojivunia - na mpaka leo lipo katika jumba la ukumbusho huko Kalenga.

## Document 4

### Lugha ya Kiswahili inavyokuza sanaa katika mipaka ya Kimataifa

*BBC Swahili, 28 Juni 2019*
*https://www.bbc.com/swahili/habari-49440711*

Kiswahili kinazidi kukua na kushamiri kila uchao na kama zilivyoenea lugha za Kiingereza,Kifaransa na Kichina, Kiswahili pia kinandelea kwenda mbali zaidi.

Juma lililopita Lugha hiyo ilitangazwa kuwa lugha ya Nne Rasmi kutumika kwa nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika, SADC

Carona Cermak, ambaye ni mwalimu wa Kiswahili katika Chuo Kikuu nchini Jamhuri ya Czech ameiambia BBC kuwa lugha hiyo imepewa nafasi kama lugha ya kimataifa.

Anasema kuwa ametafsiri kwa kiswahili mambo mengi anayofundisha.

''Naamini tukiweka mkazo kwenye kumwelimisha mtoto kupitia lugha yake mama basi atakuwa mwelewa zaidi, hivyo na mimi nikaona ni vyema mtoto wa Afrika Mashariki afaidike na haya ninayofundisha,''aliongeza Carona.

Hivi karibuni mwimbaji maarufu nchini Marekani Beyonce aliachia kibao kipya na maneno ya kwanza kabisa ya kibao hicho yalikua kwa lugha ya Kiswahili.

"Uishi kwa muda mrefu mfalme," sauti nyembamba inaimba kisha sauti nzito inaitika "uishi kwa", kionjo hiko kinajirudia mara mbili na kisha wimbo kuendelea kwa Kingereza.

Kibao hicho kiitwacho Spirit ni sehemu ya albamu inayosindikiza filamu mpya ya Lion King inayotengenezwa na kampuni kubwa ya Disney ya nchini Marekani.

Filamu ya Lion King, "inajumuisha sauti za kutoka barani Afrika," ilieleza kampuni ya Disney.

Wataalamu wanakadiria kuwa lugha ya Kiswahili kinazungumzwa na zaidi ya watu milioni 100 Duniani.

## Document 5

### Kiswahili kuwa lugha ya kikazi African Union kunafungua fursa gani kwa wazungumzaji wake?

*BBC Swahili, 15 Februari 2022*
*https://www.bbc.com/swahili/habari-60376516*

Muungano wa Afrika (African Union) umeipitisha lugha ya Kiswahili, kuwa lugha rasmi ya kikazi ndani ya Umoja huo.

Mwaka jana Shirika hilo liliitaja tarehe 7 Julai kuwa ni 'Siku ya Kiswahili Duniani"; hivyo, kuanzia mwaka huu wa 2022, kila ifikapo tarehe 7 Julai Kiswahili kitakuwa kinaadhimishwa duniani. Kwa hivyo, lugha hiyo inakuwa lugha ya kwanza ya Kiafrika iliyo na heshima hiyo.

Pamoja na kuwa Kiswahili ni lugha rasmi ya AU inayotumika katika Muungano huo, Kiswahili pia ni lugha rasmi inayotumika katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) na katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Bado Muungano wa AU unakabiliwa na changamoto nyingi za kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili itaanza kutumika katika muda usio mrefu.

Kwa mfano, linapozungumzwa eneo la nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Tanzania na, kwa kiwango fulani, Kenya, ndizo zilizo safu ya mbele.

Nchi nyingine katika kundi hilo ziko nyuma katika matumizi yao ya Kiswahili na panahitajika mkakati wa pamoja kukiimarisha kwanza Kiswahili nchini Rwanda, Uganda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Sudan Kusini ambako huko Kiswahili hakizungumzwi kabisa.

Lugha inayozungumzwa zaidi katika nchi kama Uganda ni Kiingereza. Hata Comoro ambako lugha za visiwa vyake vinne zinalingana na Kiswahili pana haja ya kukifundisha Kiswahili sanifu ili wananchi wengi wa visiwa hivyo waweze kukielewa.

Pia kumezuka mtindo wa wasomi kuzungumza Kiswahili wakikichanganya na maneno ya Kiingereza. Hili linaonekana kuanzia kwa wanasiasa kwenye mijadala bungeni hadi kwa watu wa kawaida mitaani.